

MUUNDO WA UONGOZI WA VYAMA VYA  
USHIRIKA  
(AMCOS)

MKUTANO  
MKUU( WANACHAMA  
WOTE)



BODI YA CHAMA



**WATENDAJI**

- MENEJA/MWANDISHI
- KARANI

**UFUNGUO:**



- Mamlaka



- Uwajibikaji



**JAMHURI YA MUUNGANO WA  
TANZANIA OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI  
ZA MITAA**

**USHIRIKA-PAMOJA TUJENGE UCHUMI**

**OFISI YA MKUU WA MKOA RUVUMA,** Simu  
Na: 2602256/2602238 , Fax Na: 2602144  
Anwani ya Posta: S.L.P. 74, Songea  
**Email:** ras.ruvuma.@tamisemi..go.tz  
aepe@ruvuma.go.tz

Kwa mawasiliano zaidi walisiana na Maafisa Ushirika walioko  
kwenye kila Halmashauri au Mrajis Msaidizi Mkoa wa Ruvuma  
kwa namba hizi **0754203624**

**USHIRIKA  
OFISI YA MKUU WA MKOA  
RUVUMA**

**CHAMA CHA  
USHIRIKA  
WA KILIMO  
NA MASOKO  
(AMCOS)**



## FAHAMU KUHUSU AMCOS

AMCOS ni ufupisho wa maneno Agricultural Marketing Cooperative Society ambayo maana yake ni chama cha Kilimo na Masoko.

AMCOS ni chama cha Ushirika ambacho kinaundwa na kuandikishwa kwa Shria ya Ushirika.

AMCOS ni muungano wa hiari wa wakulima wanaozalisha zao moja na wanazalisha eneo moja.

### MISINGI YA USHIRIKA

Hizi ni nguzo saba za kimataifa zinazosimamia Ushirika ambazo ni kama ifuatavyo:-

- Uanachama wa hiari na ulio wazi
- Uanachama na udhibiti wa kidemokrasia
- Ushiriki wa uanachama katika shughuli za kiuchumi
- Uhuru wa kujitegemea
- Elimu, mafunzo na tarifa

### HATUA RASMI ZA KUENZISHA AMCOS

Sheria ya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013 kifungu cha 20(1) na Waraka Namba 4 wa Mrajis wa Vyama vya Ushirika wa mwaka 2019 umeeleza kwamba watu 50 au zaidi wanaweza kuanzisha chama cha kilimo na masoko kwenye eneo la kijiji/kata na kwa kuzingatia idadi ya wakulima na uwezo wauzalishaji.

Wanachama wenye nia ya kuunda AMCOS wanapaswa kuwa na fungamanisho la pamoja (common bond) litakalobainisha mpaka wa uanachama wao ambao ni:

- Shughuli(Activity common bond) na
- Eneo la shughuli(Location common bond)

Baada ya wananchi kwa hiyari yao wenyewe kuamua kuanzisha SACCOS watatoa taarifa kwa Afisa Ushirika wa eneo linalohusika ili kupata maelekezo ya uanzishaji na uendeshaji wa Chama cha Ushirika.

### HATUA ZA UANZISHAJI

- Mkutano Mkuu wa awali
- Mkutano Mkuu wa Uanzilishi
- Mkutano Mkuu wa kupitisha masharti na makisio ya Chama
- Kuwasilisha maombi ya usajili wa chama kwa Mrajis

- Mkutano Mkuu wa kwanza:

- Uchaguzi wa Bodi ya kwanza ya Chama
- Kukabidhi hati ya Chama

### MADHUMUNI YA AMCOS

- Kuinua,kuimarisha na kuendeleza hali ya kiuchumi na kijamii ya wanachama wake
- Kuwezesha ukusanyaji nautafutaji wamasoko ya wakulima wake
- Kutoa elimu ykwa wanachama kuhusu kilimo chenye tija kinachofuata kanuni bora za kilimo
- Kusambaza pembejeo bora za kilimo kwa wanachama wake kwa bei yenye nafuu.

### MANUFAA YA AMCOS

-Kupata pembejeo bora za kilimo kwa bei nafuu

- Kupata elimu ya kilimo bora na kuweza kuzalisha mazao bora kwa kiasi kikubwa.

-Wakulima Kupata masoko ya bidhaa zao zinazozalishwa